


ITA Newsletter

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

INSTITUTE OF TAX ADMINISTRATION




Toleo Na.006/2018

December, 2018

# Mahafali ya 11 ITA yafana



*Evelyn Mwambije Mhadhiri wa Chuo cha Kodi akipokea cheti baada ya kufanya utafiti na kufanikiwa kuchapisha*

Chuo cha Kodi (ITA) kimefanya sherehe za mahafali ya 11 ambapo jumla ya wanafunzi 360 wamehitimu masomo katika kozi mbalimbali zinazotolewa na chuo hicho katika mwaka wa masomo 2017/18.

Akihutubia wanafunzi na wageni waalikwa katika mahafali hayo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt Ashatu Kijaji ambaye alikuwa mgeni rasmi amesema kwamba Chuo cha Kodi kinategemewa na serikali katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango Mkakati wa taifa wa maendeleao wa miaka mitano (2016/17-2020/21) ambao dhima yake ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu.

"Utekelezaji huu unachangiwa na shughuli mbalimbali ikiwemo uthabiti wa makusanyo ya kodi. Chuo cha Kodi ambacho ni chuo pekee hapa nchini ambacho kinatoa mafunzo ya Forodha na Kodi kinategemewa sana na serikali kuhakikisha dhana ya uchumi wa viwanda inatekelezeka kwa kutoa wataalam wa forodha na kodi", alisema Naibu Waziri Dkt Kijaji.

Amesema kwamba serikali inatambua umuhimu wa kuwepo Chuo cha kodi ambacho si tu kwamba kinatoa mafunzo kwa watumishi wa mamlaka ya Mapato pekee bali pia kwa sababu chuo kinatoa mafunzo katika taaluma ya forodha na kodi na kuwajengea uwezo wa kiutendaji wananchi mbalimbali na hivyo kuongeza ufahamu wao kuhusu masuala ya kodi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TRA Prof. Frolens Luoga

UK 2



*Kaimu Naibu Mkuu wa Chuo Utawala na Fedha wa ITA Emanuel Masalu ikipokea cheti baada ya kufanya utafiti na kufanikiwa kuchapisha*




ITA Newsletter

TANZANIA REVENUE AUTHORITY
INSTITUTE OF TAX ADMINISTRATION




December, 2018

**Imetoka Uk 1**

amesema kwamba ili chuo kiweze kufikia viwango vya kuwa kituo cha umahiri Afrika mashariki, lazima kipewe uwezo wa kupata wanataaluma wenye sifa stahiki, kiwe na uwezo wa kuwaendeleza kimasomo wanataaluma wake na kiwe na mazingira mazuri ya utendaji kazi yatakayowawezesha wanataaluma kuendelea kuwepo chuoni badala ya kutafuta kazi sehemu nyingine bora zaidi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Dkt. Samwel Werema amesema kwamba wanatambua umuhimu wa mchango wa Chuo katika kuiwezesha serikali kufikia Uchumi wa Viwanda kupitia utoaji wa elimu na ujuzi katika utozaji na ulipaji kodi hivyo Mkakati wa Nne wa Chuo unalenga kuboresha mazingira ya kazi ikiwemo miundombinu na vitendea kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika majukumu ya Chuo.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo amesema kwamba katika kutekeleza mkakati wa Nne, Chuo kitaongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiriwa hadi kufikia 1000 kwa mwaka ifikapo mwisho wa utekelezaji wa mpango Mkakati wa nne mwaka 2020/21, kuboresha ufanisi wa utendaji kwa kutumia teknolojia katika kutoa mafunzo, kuimarisha utafiti, ushauri na ubalidishanaji wa taarifa na kuendelea kujenga uwezo wa wafanyakazi wa TRA na serikali kwa ujumla katika masuala ya forodha na kodi.

Mahafali ya Kumi na Moja ya Chuo cha Kodi yamefanyika kwa mara ya pili katika ukumbi wa Chuo 'Multpurpose'na kuhudhuriwa na wageni mbalimbali wakiwemo wawakilishi kutoka mamlaka za mapato Rwanda (RRA) na Malawi (MRA) pamoja na mwakilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).



*Baadhi ya wahitimu wakifuatilia matukio katika mahafali ya 11*

Pamoja na kutunuku vyeti kwa wahitimu 360, pia zawadi mbalimbali zilitolewa kwa wanafunzi waliofanya vizuri zaidi katika masomo yao pamoja na wahadhiri sita ambao wamefanya utafiti kuhusu masuala mbalimbali ya kodi na kutoa machapisho. Wahadhiri walipata tuzo ni pamoja na Dr. Amos Ibrahim, Emanuel Masalu, Evelin Mwambije, Cyril Chimilia, Joyce Sichone, Lufina Milamo na Alfred Kimea.●



*Mgeni rasmi, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Ashatu Kijaji akizindua rasmi mahafali ya 11 ya ITA*

**Imetoka Uk 2**



*Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo, akimpongeza kiongozi wa kikundi cha Polisi cha ngoma baada ya kutoa burudani*




*Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Ashatu Kijaji (wa tatu kulia) akifuatilia burududani kutoka kwa kikundi cha Polisi cha ngoma. Wengine kutoka kulia ni; Naibu Kamishna Mkuu TRA Adolf Ndunguru, Kamishna Mkuu TRA Charles Kichere, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRA Prof. Frolens Luoga, Mwenyekiti wa Barazala la ITA Dkt. Samwel Werema, Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo na Naibu Mkuu wa Chuo cha Kodi Taaluma, Utafiti na Ushauri Dkt. Lewis Ishemoi*




ITA Newsletter

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

INSTITUTE OF TAX ADMINISTRATION




December, 2018


# ITA Chuo muafaka kufundisha watumishi TRA

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Charles Kichere amekisifu Chuo cha Kodi (ITA) kwamba ni sehemu muafaka kufundisha watumishi wa Mamlaka.

Kamishna Mkuu ametoa sifa hizo wakati wa kufunga mafunzo ya viongozi wa TRA ambayo yamefinyika Zanzibar hivi karibuni kwa awamu mbili.

"Chuo cha kodi kinatakiwa kuainisha mahitaji ya mafunzo ambayo watumishi wa TRA wanatakiwa kuyapata na kutengeneza mtaala ambao watautumia kuwafundishia", alisema Kamishna Mkuu ambaye naye alihudhuria mafunzo hayo katika awamu ya pili.



*Katibu Mkuu Utumishi Mstaafu George Yambesi akimkabidhi Kamishna Mkuu TRA Charles Kichere cheti cha ushiriki wa mafunzo ya Uongozi*




*Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala TRA Michael John (wa pili kulia) akimkabidhi Naibu Mkurugenzi wa Fedha Anna Mndeme, cheti cha ushiriki*

Amesema kwamba wakurugenzi wote wa TRA ambao hawako katika idara za ukusanyaji wa kodi wanatakiwa kuandaliwa mafunzo ambayo yatawawezesha kufahamu mambo muhimu yanayohusu ukusanyaji wa kodi. "Wakurugenzi hawa wanatakiwa kuwa na uelewa wa jumla wa masuala ya kodi", alisema Kichere.

Adiha alisifu uamuzi wa ITA kumtumia Katibu Mkuu Utumishi Mstaafu George Yambesi kuwa mmoja kati ya watoa mada katika mafunzo hayo kwa kusema kwamba ni vema kuwatumia wazoefu katika utumishi wa umma ili kuwapatia viongozi wa TRA misingi mizuri ya utumishi na kuwapatia undani wa dhana ya weledi, uwajibikaji na uadilifu.

Katika mafunzo hayo, wakuu na manaibu wakuu wa idara zote za TRA walipatiwa mafunzo ya uongozi ambayo yaliandaliwa na Idara ya Utawala na rasilimali watu na kuratibiwa na Chuo cha Kodi.●




Imetoka Uk 4

# ITA Newsletter

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

INSTITUTE OF TAX ADMINISTRATION








*Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo akimkabidhi Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawlaa TRA Michael John cheti cha kushiriki mafunzo ya uongozi*

Baadhi ya mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na misingi ya maadili kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi Mstaafu George Yambesi, na uthibiti wa muda, mabadiliko na utekelezaji wa malengo somo ambalo lilitolewa na Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo.



*Kamishna Mkuu TRA Charles Kichere (waliokaa katikati) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa awamu ya pili ya mafunzo ya Uongozi kwa viongozi wa TRA*





ITA Newsletter

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

INSTITUTE OF TAX ADMINISTRATION

December, 2018





# Dkt Ishemoi awaambia wanafunzi wapya, 'Zingatieni masomo'



*Baadhi ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa masomo 2018/19 wakimsikiliza Naibu Mkuu wa Chuo cha Kodi taaluma, Utafiti na ushauri Dkt. Lewis Ishemoi (hayupo ktk picha)*

Wanafunzi wapya wa masomo mwaka 2018/19 wamehimizwa kuzingatia masomo katika kipindi chote wawapo katika Chuo cha Kodi pamoja na kuutumia uhuru walionao kwa manufaa yao wenyewe.

Ushauri huo umetolewa na Naibu Mkuu wa Chuo cha Kodi Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi Dkt Lewis Ishemoi wakati akiwakaribisha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na masomo chuoni hapo mwaka 2018/19.

"Maisha ya Dar es salaam na uhuru katika Chuo vinaweza vikawapotezea fursa za masomo. Jitahidini kuwa na tabia nzuri kama mlivyotoka majumbani kwenu", alisema Dkt. Ishemoi na kuwaasa wanafunzi hao kuepuka vitendo vya kitapeli, kujiepusha na magonjwa hususan Ukimwi pamoja na magonjwa mengine na kusisitiza, Ukimwi upo".

Aliwafahamisha wanafunzi hao kwamba Chuo kinataratibu kilizojiwekea ili kufanya maisha katika Chuo kuwa mazuri hivyo ni wajibu wao kuzifuata na kupaona chuoni kama mahali pazuri pa kuishi na kusoma.

Dkt Ishemoi alisema, "Wale watakaosoma watafaulu, watakaoshindwa kusoma watafeli".

Aidha aliwakaribisha katika maisha mapya katika chuo na kuwashauri kupata msaada kwa walimu au watumishi wa chuo wakati wowote wakihitaji msaada.

Jumla ya wanafunzi 433 wamechaguliwa kujiunga na Chuo cha Kodi katika programu mbalimbali zinazotolewa na chuo katika mwaka wa masomo 2018/19.

Kati ya hao PGDT ni wanafunzi 57, BCTM, 158, DCTM 161, CCTM 33 na CFFPC 58.●



*Naibu Mkuu wa Chuo cha Kodi Taaluma, Utafiti na Ushauri Dkt. Lewis Ishemoi akisisitiza jambo wakati akiwakaribisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa masomo 2018/19. Wengine katika picha kutoka kulia ni Hamida Msofe,Naibu Mkuu Taaluma Shirikishi Philp Mbati Mkuu wa Taaluma ya Kodi na Ryoba Mzalendo Mkuu wa Mipango na Mifumo*




ITA Newsletter

TANZANIA REVENUE AUTHORITY
INSTITUTE OF TAX ADMINISTRATION




December, 2018


# Watumishi wa Chuo cha Kodi watakiwa kutoogopa mabadiliko



*Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo akifafanua jambo wakati wa semina kwa watumishi wa Chuo cha Kodi*

Mkuu wa Chuo cha Kodi (ITA) Prof. Isaya Jairo amewataka wafanyakazi wa Chuo hicho kwenda na wakati katika maisha pamoja na kutumia teknolojia kwa manufaa yao.



*Baadhi ya watumishi ITA wakifuatilia mada wakati wa semina*

Prof. Jairo ametoa wito huo wakati akifunga semina kwa watumishi wa chuo hicho ambayo imefanyika Morogoro hivi karibuni.

"Tukubali kubadilika kwa sababu ulimwengu unabadilika kwa haraka sana", alisema Prof. Jairo na kuongeza kwamba wafanyakazi wanatakiwa kuwahi na kuwepo mahali pa kazi muda wote wa kazi.

Amesema kwamba kwa sasa ulimwengu unashuhudia mabadiliko makubwa na ukuaji wa teknolojia hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuzitumia teknolojia kwa manufaa yake na taifa kwa ujumla.

Akitoa mfano wa mabadiliko katika mifumo ya ufundishaji, Prof. Jairo amesema kwamba wakati ukifika wa kutumia mifumo bora ya teknolojia katika ufundishaji lazima wote wanaohusika kuhakikisha wanaielewa na kuitumia mifumo hiyo ili wasibaki nyuma.

Awali akiwasilisha mada kuhusu uthibiti wa muda, mabadiliko na utekelezaji wa malengo, amesema kwamba ni lazima kuepukana na tabia ambazo zinapoteza muda na kuutumia muda vizuri kuongeza ufanisi na tija ili kufikia malengo ambayo kila mmoja amejiwekea.

Amewasisitizia watumishi hao umuhimu wa kujiwekea malengo pamoja na kubuni mikakati itakayowawezesha kuyatekeleza kwa ufanisi.

Katika semina hiyo ya siku mbili, wafanyakazi hao wamepata mafunzo mbalimbali ikiwemo, uelewa wa magonjwa ambayo hayaambukizi, Maadili pamoja na Mkakati wa Nne wa Chuo cha Kodi.




ITA Newsletter

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

INSTITUTE OF TAX ADMINISTRATION




December, 2018

# Kamishna Mkuu atembelea Chuo cha Kodi

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Charles Kichere ametembelea mazingira ya Chuo cha Kodi pamoja na kuongea na uongozi wa Chuo ikiwa ni ziara yake ya kwanza tangu ateuliwe kushika wadhifa huo mwaka 2017.

Katika ziara hiyo, Kamishna Mkuu aliambatana na Naibu Mkurugenzi wa Utumishi Bi Alice Lukindo ambapo kwa pamoja walitembelea Ukumbi wa Multipurpose, maabara ya kompyuta, chumba cha mazoezi ya viungo, maktaba, jikoni, mabweni pamoja na madarasa.



*Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo (wa kwanza kulia) pamoja na baadhi ya viongozi wa ITA wakiongozana na Kamishna Mkuu wa TRA alipokitembelea Chuo*

Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Jairo amemueleza Kamishna Mkuu baadhi ya changamoto ambazo Chuo kinakabiliana nazo katika kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo kwa watumishi wa TRA pamoja na wadau wengine wa masomo ya muda mrefu.



*Kamishna Mkuu akisikiliza maelezo ya Huduma za Mkataba kutoka kwa Mkuu wa Huduma za Mkataba Ibrahim Mshigati*

Pamoja na kwamba ziara hiyo hakuipanga, Kamishna Mkuu alimshukuru Mkuu wa Chuo kwa kumtembeza katika maeneo mbalimbali ya Chuo ili kuweza kufahamu changamoto zinazokikabili chuo na jinsi ya kuzishughulikia.

Pia aliwapongeza watumishi wa Chuo kwa jitihada zao katika kuhakikisha mafunzo yanatolewa na kuwataka kuhakikisha wanatoa mafunzo yatakayoisadia mamlaka kukusanya kodi kwa weledi.●



*Kamishna Mkuu akiangalia mojawapo ya machapisho katika makatába ya ITA*











**Imetoka Uk 4**



*Kamishna Mkuu akiwa katika mojawapo ya madarasa ya ITA. Wa kwanza kushoto ni Naibu Mkurugenzi Utawala Alice Lukindo*



*Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo, akitoa maelezo kuhusu vyumba vya kulala wanafunzo wa ITA*



*Mkuu wa Miliki za Chuo Joyce Mwaifuge akimuelezea Kamishna Mkuu kuhusu ukarabati wa jiko na sehemu ya kula chakula wanafunzi*




*Kamishna Mkuu akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo alipokutana na uongozi wa Chuo katika chumba cha Baraza la Chuo baada ya kutembelea sehemu mbalimbali za chuo*




ITA Newsletter

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

INSTITUTE OF TAX ADMINISTRATION




December, 2018

# Majaji wa Mahakama Kuu Malawi wapata mafunzo ITA

Mojawapo ya majukumu ya Chuo cha Kodi (ITA) ni kutoa mafunzo ya muda mfupi sio tu kwa watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) bali pia kwa wadau wengine ndani na nje ya nchi.

Katika kutekeleza jukumu hili Chuo cha Kodi kimeendesha kozi fupi kuhusu mada mbalimbali za masuala ya forodha na kodi kwa watumishi wa TRA, watumishi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na kwa watumishi kutoka Malawi.

Jumla ya watumishi sita kutoka Malawi walipata mafunzo katika utozaji wa kodi za kimataifa kwa muda wa wiki mbili.




*Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo akiwakaribisha na watumishi wa Malawi kabla ya kuanza kwa mafunzo yao*

Watumishi ambao walipata mafunzo kupitia kozi fupi kutoka Malawi ni pamoja na Majaji wawili wa Ma-



*Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo akizungumza na watumishi wa Malawi kabla ya kuanza kwa mafunzo yao*

**Katika kutekeleza jukumu hili Chuo cha Kodi kimeendesha kozi fupi kuhusu mada mbalimbali za masuala ya forodha na kodi kwa watumishi wa TRA, watumishi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na kwa watumishi kutoka Malawi.**




*Kamishna wa Walipakodi Wakubwa Alfred Mregi akimkabidhi cheti mtumishi wa TRA baada ya kuhitimu mafunzo ya Transfer Pricing*

hakama Kuu, msajili wa Mahakama Kuu pamoja na wanasheria wawili wa mamlaka ya Mapato Malawi (MRA).

Pamoja na kozi hizo fupi Chuo cha Kodi pia kimeratibu na kuendesha kozi fupi kwa watumishi wa Bodi ya Mapato Zanzibar ikiwa ni utekelezaji wa makubaliano ya kuwajengea uwezo watumishi wa ZRB.●



*Baadhi ya washiriki wa kozi wakifuatilia maelezo ya ufungaji wa mafunzo*



*Washiriki wa kozi ya kupambana na uhalifu katika picha ya pamoja baada ya kumalizika kwa kozi*

# ITA, TAFFA kuendelea kushirikiana

Chuo cha Kodi na Chama cha Mawakala wa Forodha Tanzania (TAFFA) wametiliana saini makubaliano ya kuendelea kushirikiana katika usimamizi wa mafunzo ya Cheti cha Uwakala wa Forodha Cha Afrika Mashariki (EACFFPC).

Makubaliano hayo yamefanyika katika ofisi ya Mkuu wa Chuo cha Kodi Dar es salaam hivi karibuni na kushuhudiwa na baadhi ya maofisa wa TAFAA pamoja na Mkuu wa Mafunzo ya Forodha ITA Edward mwakimonga na Mkuu wa Usajili wa wanafunzi ITA Justin Musa.



*Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo akisaini hati ya makubaliano kushirikiana na TAFFA kusimamia mafunzo ya cheti cha Uwakala wa Forodha*

Kwa mujibu wa hati ya makubaliano, taasisi hizo mbili zitasimamia mafunzo ya EACFFPC pamoja na maendeleo ya mafunzo ya taaluma katika fani ya uwakala wa forodha kwa wadau wa TAFFA ikiwemo ushauri wa kiufundi.



*Mkuu wa Chuo cha Kodi Prof. Isaya Jairo na Rais wa Chama cha Mawakala Tanzania (TAFFA) Stephen Ngatunga katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi wa ITA na TAFFA mara baada ya kusaini makubaliano kushirikiana kusimamia uendeshaji wa mafunzo ya cheti cha Uwakala wa Forodha*

Majukumu makubwa katika kipindi cha utekelezaji wa makubaliano hayo ya miaka mitatu ni pamoja na kuundwa kwa kamati ya taifa ya kutekeleza mtaala ambayo itasimamia mtaala wa EACFFPC kwa kuzingatia viwango vya ubora wa mafunzo.

ITA imekuwa ikishirikiana na TAFFA kuendesha mafunzo ya Cheti cha Uwakala wa Forodha ambacho kinatambuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo wahitimu wa mafunzo haya wanaweza kufanya kazi za uwakala katika nchi yoyote mwanachama wa EAC.●